# HAWAOMBI VYAKUTOSHA

*Wakolosai4:2-4, Dumuni sana katika kuomba, mkikesha katika Kuomba na shukrani;mkituombea na sisi pia,kwamba Mungu atufungulie mlango kwa lile Neno lake, tuinene Siri ya Kristo,ambayo kwa ajili yake Nimefugwa, Ili nii dhihirishe kama inipasavyo kunena.*

Sikiliza kile nabii wa Mungu alicho sema juu ya hilo**:**

Unajua,tunaweza tukaimba sana.Tunaweza kupiga makelele sana mpaka tuishiwe na sauti zipwelee.Na tunaweza kuimba/kupiga makele wakati ambao sio,lakini hapa pana jambo moja ,kamwe hatuwezi kuwa nje ya utaratibu;wakati tunapoomba. [1]

Maombi yanabadilisha mambo.Maombi yanabadilisha kifo kuwa uzima.Maombi yana badilisha ugonjwa na kuwa mwenye afya, yana badilisha wenye dhambi kuwa watakatifu. Ni maombi. Unaweza ukacheka kupita mpaka.unaweza ukapiga makelele sana.unaweza ukala sana. Lakini huwezi kuomba sana. Biblia ilisema,’’Basi nataka wanaume wasali kila mahali, wakiinua mikono iliyo takata``(1Tim,2:8).Kwa hiyo huwezi kamwe kuomba sana. [2]

Baba, ni fulsa iliyo kuu sana mwanadamu aliyowahi kupata ni kufunga macho yake, na kufungua moyo wake,na kuzungumza na Wewe. Na tunajua ya kwamba wewe unasikia, kama tunaweza kuamini kuwa wewe unasikia.kwa maana Yesu alisema, “kama mkimwomba Baba jambo lolote kwa Jina langu hilo nitalifanya.”Hilo ni kwa sharti kwamba hatutaona shaka yoyote(Mark11:24-25). [1]

Nalipenda Neno, oh natamani kama ningeweza kulidhihirisha hilo.Unajua mahali ambapo ninahubiri mahubiri yangu mazuri? Ni katika chumba changu cha maombi nyumbani au mahali fulani, kitandani. Ninalala usiku na kupakwa mafuta kwa Roho Mtakatifu; ninajihubiria mwenyewe nusu ya usiku wote.Oh kama ningeweza kufanya hivyo mimbarani, lakini ninakuwa na haraka, mbio mno, na kidogo ninajitangulia mbele mwenyewe.Nafikiri hivyo ni kwa ajili ya kukosa utulivu, na kupotewa na mawazo.Lakini mnisamehe hilo ni….

Je hupendi kuwa peke yako na Bwana? Oh jamani jamani,kule kuwa peke yako. Kuna wakati….tumezoea kuimba wimbo mdogo, “kunawakati napenda kuwa peke yangu na Kristo, Bwana wangu,”uliwahi kuusikia huo?Ninaweza



kumwambia matatizo yangu yote tunapokuwa peke yetu. Na ndiyo namna anayotaka kukupata wewe, peke yako na Yeye. Maombi yako, sio hasa wakati unapokuwa, oh, pengine umekuja, unajua, kwa mfano uwe, vema, katika kundi la hadharani unaomba kama kanisani au kuzunguka madhabahu, kuwa peke yako,utaomba maombi ya tofauti. Unapokuwa peke yako kuliko unapokuwa hadharani kaa peke yako, ninyi nyote, nenda mahali pako na uwe na mkutano halisi wa siri, ambapo wewe na Bwana mnakutana mara kadhaa kwa siku na unaomba(Luka22:39-46;12;9;p18).

Wahubiri/mhuduma, kwa nini hatuna mzigo kwa nafsi zilizo potea.Naamini ni kwasababu ya kukosa uamsho.Naamini inabidi bado tujaribu kuomba Mungu atupe shauku kwa nafsi zilizo potea mpaka Yesu atakapo kuja. [4].

Na, kumbuka, yule mwanaanga anatawaliwa na nguvu ya rada. Mliwaona walivyomleta John Glenn ndani.Niliangalia kwa chini pale kule Cape Canaveral na kuona ile rada kubwa,na usingeweza kumuona yeye popote,lakini ungeweza kusema mahali alipo kwa kutumia rada ilikuwa inaelekeza.Pale ndipo alipokuwa. Unaona? Na sisi pia tunayo rada pia:Maombi.Maombi ni nguvu ya rada inayo tuelekeza yule mwanaanga.“mwombeni Baba chochote kwa jina langu; nitalifanya.Unaona? Wewe angali tu yale maombi yanakoenda, unaweza ukajua njia anayoelekeza. Amina.angalia tu vile kanisa linavyoomba, unaweza uone kule ambako virusha silaha (missile) vina rushia. Unaweza kueleza hilo kwa namna ambayo mwana anga anasafiri, kwa namna ambayo kanisa linaomba. [5].

Na sasa,nawashukuru ninyi kwa kuniombea mimi. Nilijua wengi wenu wangeniombea, kwa kusikia kwamba nimeumia. Na kundi moja dogo ambalo lime….Binti yangu nyuma pale, Rebeka, alimwandikia barua Dada Dauch ambaye anakuja hapa kanisani na kumuambia juu ya hilo. Na akampigia simu Meda usiku, baada ya hilo akasema, “sijui kama ilisaidia au la, lakini kundi la sisi sote tulikusanyika pamoja.” mhuduma wa Methodist, na ndugu Brown, na ndugu zao na wote wakakusanyika pamoja, wakaomba usiku mzima kwa ajili yangu. Akasema, sijui kama Mungu alisikia au la, lakini tulijua ndugu Branham anaombea wengi; tuliwaza tungemwombea yeye “Hao ndio Yeye ambao anawasikia, (unaona?ndio, Bwana!) wale wa aina kama hiyo.

Ndugu Crase,mmoja wa ndugu zetu hapa,shetani alimfuata hivi karibuni, aligonga kalvati, oh, lilitaka…..kabisa. Sielewi jinsi alivyo toka pale akiwa hai.Kwa hiyo alikuwa ame lala pale hospitalini na akasema alikuwepo ndugu mdogo kutoka New Albani, anaitwa Metcalf naye akasema, ndugu Crase, sistahili kuja kukuombea wewe, lakini akasema Bwana ameliweka kwenye moyo wangu, kiasi kwamba siwezi kujisaidia.Na akaja

pale
na kupiga magoti na kufanya maombi madogo na akaenda zake, Mungu alimponya ndugu Crase pale pale.Unaona?Lakini unaona, ni kipawa cha uponyaji katika mwili wa Kristo, kutoka mshirika mmoja kwenda kwa mwingine. (1Kor.12:4-11;14-27).

Usifikirie kwamba eti kwa sababu ni mshirika wa kawaida kuwa….wewe ni mshirika tu kama mshirika mwingine.Hiki ni kidole changu kama vile mkono huu ulivyo mkono wangu au hili sikio ni sikio langu. Unaona? Ni mshirika tu wa mwili.Kama mshirika mmoja akiteseka, washirika wote wanateseka pamoja naye (1Kor.12:26) umoja, jinsi umoja ulivyo barikiwa. [6]

Si kitu cha ajabu kwamba Mungu anataka wote wawe na sehemu katika hilo? Yesu aliangalia katika mavuno, Alisema, "mavuno yameiva; watenda kazi ni wachache.mwombeni Bwana wa mavuno(Ambaye ni Yeye)---Niombeni mimi, ili nipeleke watenda kazi katika mavuno yangu" (Matayo 9:36-38).Kuna sehemu upaswayo kufanya.Mungu analisubiri kanisa lake limuite/limuombe Yeye (Rumi10:12-13). Siku zote amefanya hivyo, Mungu anasubiri leo watu wamwite ili watumishi wake waingie kazini.Na watumishi hawawezi kuingia kazini mpaka watu waombe.

Israeli hawangeweza kuingia katika vitendo kwa ishara na miujiza mpaka kwanza watu waanguke nyusoni pao waombe kupata mkombozi. (Kutoka 3:6-8). Mungu alikuwa na Mkombozi wake. Mungu alikuwa na Nabii wake aliyekuwa kule jangwani, alimweka pale miaka arobaini akiwangojea wawe tayari kuomba. lakini walipokuwa tayari na kuanza kuomba, hapo sasa Mungu alimtuma Mkombozi. Mungu atafanya jambo hilohilo leo, kama watu watakusanyika pamoja, waanze kuomba.Vema.kwanza lazima waombe. Mungu anasubiri.
[7]

Mungu analeta jibu kwa maombi yako:Umeomba,na hivyo utapokea.Ninaweza kusimama hapa kwa masaa juu ya wanaume na wanawake, ambao ni wakristo, waliomba juu ya jambo fulani; na Mungu anawapa jibu na hata hawatambui hivyo.

Na sasa, Mungu amewapa jibu. walikuwa wanahitaji Mesiya. walijua wanaye kaisari, na wamekuwa na Daudi; wamekuwa na Sulemani mtu mwenye hekima; wamekuwa na akina Daudi mashujaa wa vita; wamekuwa nao aina kwa aina; lakini walijua wanahitaji msaada utokao mbinguni na wali…..Mungu aliwaahidia kupata Masihi. Na akamtuma yule masihi akiwa ni jibu kwa maombi yao, lakini hawakumtaka Yeye (Daniel 9:25-26 Yohana19:15; Yohana1:11)

Nashangaa leo, kama majibu yetu…Unawasikia wao wakisema, omba



kwa ajili ya uamsho mkuu, omba kwa hili. Omba tufunguliwe vikwazo vyote.Omba kwa umoja, Nashangaa kama Mungu atatuma huo utaratibu, kama tutaukubali huo. Nashangaa kama kweli tutakikubali kile anacho tutumia sisi. Sababu inayofanya tuombe mambo haya ni kwa sababu tunajua yanahitajika.

Lakini wakati Mungu anapolituma katika njia ambayo Yeye anataka, hapo sasa inakuwa sio sawa na radha yetu, na kwa hiyo, hatuwezi kulipokea hilo, na hivyo ndivyo ilivyokuwa katika siku ile.Kama hakuwa katika ladha yao na imani yao na…..hata leo hawawezi kumpokea tena.Ndio maana waliuliza hili swali, huyu ni nani? Ni nani mtu huyu anayekuja?
[8]

Ishara inayorukwa, ishara ya kweli, na wanaikosa hiyo.Sikuzote hufanya hivyo.Kurudi kwenye kanisa la kweli, kwenye ujumbe wa kweli.
[9]

Yesu alisema,chochote mmwombacho Baba kwa Jina langu, hilo nitalifanya (Yohana 16:23) Je ulitambua hilo lina maanisha nini? Unatambua kwamba tunapo mwomba Mungu kwa Jina la Yesu, ni sawa tu na Yesu mwenyewe akiomba? Sio mimi tena ninaye omba. Kama ninakuja katika Jina lake, na analitambua Jina lake, na Yesu alisema, chochote mmwombacho Baba kwa jina langu, hilo nitalifanya. Na halafu ninamwendea Baba kwa Jina la Yesu, siyo mimi tena ninaye omba; ni Yesu. Ni Roho wake anayeomba kupitia mimi (Rumi 8:26-27)

Halafu inabidi nipokee kile ninachoomba, kwa sababu alisema hilo na ni Neno la Mungu mwenyewe. Haliwezi kufanya vinginevyo. Litatenda kama lilivyosema.

Kwa hiyo tunaamini kuwa tu…..Huu ndio uhakika tulio nao kwa Mungu kwamba tunapata kile tuombacho, kwa maana Yeye ni Mungu na hawezi kuondoa (alicho kwisha sema). Neno lake. Lazima ashike Neno lake-(1Yohana 3:21-22)

Kwa hiyo sasa,ukikaa ndani yangu na Maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo, nanyi mtapewa (Yohana15:7). Hilo si rahisi? Imani iliyo umbwa. Tumeumbwa kwa kusudi hilo. Halafu kupitia anguko, kwa nini, tumechukuliwa mbali na hilo, na halafu katika ukombozi tumerudishwa tena katika hilo. [10]

Mtu fulani alisema "mnamuomba nani? nilimuombea mtu fulani na fulani kuhusu jambo fulani; sikulipata hilo "nikasema, unaomba vibaya. Kamwe hatupaswi kuomba kubadilisha mawazo ya Mungu; tunapaswa kuomba kubadilisha mawazo yetu. Mawazo ya Mungu hayahitaji kubadilishwa. Yako sahihi" nikasema, "siyo yale unayo yaomba…..

Ninajua kijana mkatoliki wakati mmoja alikuwa na kitabu cha maombi

akisema maombi ili mama yake aishi. Naye akafa, akakirusha kile kitabu cha

maombi katika moto. Vema, unaona….Sitetei kitabu cha maombi lakini iwavyo vyote…Unaona, unachukuwa msimamo ambao sio sahihi.Unajaribu kumuambia Mungu jambo la kufanya. Maombi yanapaswa kuwa, "Bwana, nibadalishe mimi nilingane na Neno lako,"siyo kubadilisha siyo, "Niache mimi nibadilishe mawazo yako".Badili mawazo yangu. Badili mawazo yangu yaje kwenye mapenzi yako, na mapenzi yako yameandikwa hapa katika kitabu. Na Bwana,usiniache niende mpaka umeyaweka mawazo yangu kuwa kama yako. Na mawazo yangu yatakapokuwa kama yako hapo sasa nitaamini kila Neno ulililoliandika. Na umesema pale kwamba utalifanya kila Jambo litende kazi kuwapatia mema wale wakupendao, na nina kupenda, Bwana. Inatenda kazi kunipatia mema, (Rumi 8:28-29).
[11].

Unajua, wakati mwingine tunapokuwa tunaombea wengine, sisi wenyewe mara nyingi ndio tunapata msaada wakati unapoombea wengine.
[12]

" Sasa, Yesu, hakusema, wekeni mikono muombe".Alisema, ishara hizi zitaambatana nao waaminio,kama wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa. (Marko16:17-18). Kamwe hakusema, tuwaombee; kuweka tu mikono juu yao. Huo ndio utaratibu wa kuomba ulivyo"waite wazee wa kanisa, na wawapake mafuta halafu wawaombee (Yakobo5:14-16) hiyo ni kwa ajili ya kanisa.Lakini kipawa cha kiinjilisti cha kuponya ni kuweka mikono juu ya wagonjwa. Tunajua hilo. Siyo kuwaombea wao, ni kuweka mikono juu yao, ishara hizi zitafuata. [13].

Ndugu Branham aliulizwa: "Tuambie sisi tunaweza kufanya nini kwa ajili yako ili kukupunguzia mzigo". Sasa, hilo sitamu. Unaona?

Tunaweza kufanya nini kupunguza mzigo? Ndio, ndugu, dada yoyote yule aliyeandika hili, Niombee mimi; hicho ndicho kitu kizuri zaidi cha kufanya. Asante. Sihitaji fedha, Ni………. Zinakuja za kutosha kunihudumia. Namshukuru Bwana kwa hilo. Sihitaji nguo. Wakati mwingi watu hunipa nguo zangu ninazo vaa. Na marafiki zangu na vinginevyo hunipa nguo zangu. Na ninapata fedha za kutosha kulisha familia yangu; hivyo ndivyo vyote tunavyo hitaji msaada wa kiroho.
[14]

Kwa hiyo kama maombi ya Imani yanaleta baraka za Mungu kwetu, Natuendelee kuomba. [15]

Nami nilikuwa nasikiliza haya, huyu kijana mdogo na huyu mwingine hapa, akiomba muda mfupi uliopita, kwa shauku kubwa. Niliwaza,--"unajua nilikuwa ninaweza kuomba kama hivyo, bila kukamata pumzi hasa, Na



halafu unakuwa umezeeka, unaanza kupungua chini kidogo, unajua, hilo. Bado unaendelea, lakini uko kwenye gea namba mbili kama nilivyomwambia ndugu wood nje kule. Na baada ya muda unaenda chini tena katika gea ya chini, Unapokuwa na umri wa miaka sabini au themanini, nadhani. Lakini, unajua, bado unaendelea. Ili mradi unaweza kuendelea kutembea, haifanyi tofauti au sio? Muda mdogo tu zaidi kufika pale.
[16]

Yesu katika nyumba ya yairo hakuwa nahaja ya kuomba (Marko 5:21-24,35-45); Yeye alikuwa Neno. Sina haja ya kuomba kama ninaweza kuona ono, "kwa sababu Neno limeshafanywa tayari.(lipo). Ninapaswa kuomba ili kulipata Neno, kujua kile Mungu anachosema, halafu sasa nina Nena hilo, baada ya kupata Mungu anachosema. Lakini Yeye alikuwa ni Neno Amen!
[17]

Sasa, katika maandiko kulikuwa na mtu anaitwa Jehoshaphat, mtu mkuu, mtu wa kidini, Na akaenda kwa mfalme mwingine, ambae alikuwa mfalme wa lsraeli.
Na yeye, Jehoshaphat akiwa ni mfalme wa yuda, na aliendа kwa Ahabu mfalme wa lsraeli, nao wakafungamana pamoja na wakafanya umoja kwa mwingine ili kwenda kupigana kule Ramoth-gileadi. (1Wafalme 22:1-38). Na walifanya hivyo bila ya kuomba kwanza.

Oh, kama watu wangeweza kutambua. Hiyo ndiyo maana nimekuja asubuhi hii ya leo na ninaomba mnikumbuke mimi ninapoenda nchi za nje.. Katika mambo yote, Ombeni. Mtu mmoja alikuja siku moja na kusema, "Ndugu Branham, unafikiri ni vibaya kufanya jambo fulani?" Nikasema, "kwa nini unajiuliza swali juu ya hilo?" unaona? Kama kuna swali akilini mwako, liache hilo usilifanye kabisa kaa nalo. Unapoanza kufanya chochote, na kama kuna swali na kama ni sahihi au siyo, kaambali nalo usiende katika hilo kabisa. Hapo sasa unajua uko sahihi.

Sasa mambo yote yapaswa yaamuliwe kwa maombi kwanza. "Utafuteni kwanza ufalme wa Mungu na hali yake na haya yote utazidishiwa"(Matayo 6:33-34)
Ninao uhakika asubuhi hii ya leo kama wanaume na wanawake watafika mahali ambapo Nafsi zao, mawazo yao, mitazamo yao itakuwa mikamilifu mbele za Mungu. Hili litakuwa kanisa lenye nguvu lililowahi kuwapo.
[18]

Nataka niwape siri ndogo. Mungu amenibariki sana, na yeye nina mpa utukufu/sifa, katika kuombea wagonjwa. Na nimeliona hilo katika miaka hii yote, na nimejua ni ukweli kabisa. Siwezi kamwe, kufanikisha maombi yangu mpaka kwanza niingie kwenye ushirika na hao watu ninaowaombea. Lazima niingie katika hali ya yule mtu vile anavyojisikia.

Sio muda mrefu uliopita hapa, kule meksiko, maskini mmeksiko mmoja, mweusi, nywele zenye mvi, na ndevu zake zinamvi, kamwe pengine hajapata mlo mzuri maishani, na akaja mimbarani, yeye ni mkatoliki kwa imani, akiwa anatembea na kofia ndogo juu yake, hana viatu, miguu yake imesinyaa. Alikuwa ananiulizia mimi. Na alipopiga magoti mbele zangu, nilimuinua kwa mikono yangu, naye akawa anatafuta rozari yake, na ilikuwa rozari ya zamani kukuu, alikuwa anazisugua sana kusema maombi yake. Na nikamwambia, "Hiyo sio ya lazima, baba. Nataka wewe umwamini Bwana Yesu"

Na akainua mikono yake mzee juu; akayashikilia mabega yangu, na akaigamisha kichwa chake hapa mabegani. Nikaangalia chini ile miguu iliyo sinyaa, vumbi, michafu. Nikavua viatu vyangu kuona kama vitamtosha yeye. Nilikuwa radhi nitembee miguu tupu kuliko kumuona akitembea hivyo. Unaona, na moyo wangu ukamuelekea yeye; alikuwa ni kipofu (Yakobo 2:13)

Sasa, hapo ndipo unapoingia katika hilo. Taratibu zetu zote zitashindwa. Ishara zetu zitashindwa. Karama zetu zote zitashindwa lakini Upendo kamwe haushindwi (1korntho13:4-7). Hilo ndilo linalohitajika ili kushikilia.

Na nikafikiri, maskini mzee huyu, umri karibu sawa na Baba yangu angekuwa anaishi. "Na nikafikiria, pengine na yeye ana mtoto mahali fulani". Na alikuwa akizungumza kwa kuuma uma jambo fulani, na yule mtafsiri hakuniambia hilo. Na nikamuangalia yule mtu mzee. Na nisingeweza ku……… Siyo katika macho yangu, lakini katika moyo wangu. Nilikuwa natamani hata matone ya machozi yatoke. "maskini, "mzee, huyu", Nikafikiri, pengine hajapata mlo mzuri katika maisha yake, alikuwa hana uzuri. Na nikaingia katika hali ile pamoja naye; nikaingia katika mateso yake.

Nikawaza pamoja na kuwa maskini, pamoja na hali yake na magonjwa yake, yote hayo, katika dunia ya giza, haoni; kipofu. Nikawaza, oh Mungu, ni vipi kama huyu angekuwa ni Baba yangu amesimama pale? Halafu nikawa najisikia vile alivyo. Nikasema, "Baba wa mbinguni mhurumie mtu huyu kipofu.

Haikuwa kuomba kupitia kichwa changu. Ilikuwa ni kitu fulani moyoni kikiomba hilo. Unaona? Lakini Upendo………

Nami nikamsikia akiondoka. Na pale wameksiko, maelfu kwa maelfu walikuwa wakilia kwa kupiga kelele. Nikashangaa ni nini alikuwa akilia, ninaona ninaona" Halafu akageuka nyuma na kupiga magoti chini na kuanza kunisugua viatu vyangu, akinipigapiga miguuni, nami nikamwinua juu. Naye akakimbia juu na chini mzee huyu aliye zeeka akisema, "Ninaona, ninaona".

Ilikuwa ni nini? Kuingia kwenye ushirika naye.



Upendo, huo ndio ufanyao hilo, siyo kujitesa, ni uUpendo safi usiochanganyika. Utashinda karama zote za kuwekea mikono, utashinda tafsiri zote na kunena kwa lugha. (1korintho13:8-13)

Hiyo itashinda vyote vya……… Ningesema, sauti zote nzuri za kuimbia. Itashinda kila kitu, kama utaingia kwenye Upendo wa Mungu na mtu yule ambae unajaribu kumleta kwa Bwana Yesu. Na unaenda kumsoma huyo rafiki yako aliyepotea mpaka huwezi kustahimili mchana na usiku, inabiddi tu umuendee kwa Upendo. Angalia kile Roho Mtakatifu atakacho kifanya. Upendo wa Mungu unatuhimiza sisi (2korintho 5:14)

Hivyo ndivyo mkristo halisi anavyofanya. Unaomba na kujinyenyekeza mwenyewe, na kukaa mbele za Mungu mchana na usiku ili uweze kujitolea kwa ajili ya mtu mwingine. [19] Kama vile tuu nipendavyo mtu mwingine ashikilie na kuomba kwa ajili yangu ninapopitia majaribu yangu, na unataka mtu fulani kwa ajili yako.[20]

Siyo kile unachoweka, ni kile unachotoa ndicho kinacho hesabika. Lazima ujitoe mwenyewe kwa ajili ya wengine. [19]

Na siwezi nikampenda Kristo mpaka kwanza niwe ninawapenda watu wake. Unaona? Nilazima niwapende watu wake. Kwa hiyo nawapenda watu wake, Hivyo ninampenda Yeye (1Yohana3:14-18; 4:7-13).
[20]

Leo watu wanatembea bila kujua; hawajui kwamba hili Neno ni kweli. Wanafikiri ni kama uzushi fulani. Hawaingii ndani vya kutosha, katika roho ya ufunuo. Hawaombi vya kutosha; hawa muiti Mungu vyakutosha. Wanayachukulia kiwepesiwepesi, "oh naamini ni Mungu. Hakika". Shetani anaamini jambo hilohilo. Shetani anaamini zaidi ya watu wengine wanavyodai kuamini; Shetani anaamini hilo na kutetemeka(Yohana 2:19) Watu wanaliamini na kuendelea, lakini shetani anatetemeka, akijua hukumu yake inakuja. Na watu wanaliamini hilo na hawajali kuwa hukumu inakuja.
[22]

Roho Mtakatifu haonekani kuwa na haki katika kanisa zaidi ya kitu chochote. Hakuna tena mikutano ya maombi, hakuna kuugua kumsihi Mungu atimize Neno lake. Hawaamini tena lile Neno kuwa Yeye yule jana leo na hata milele. [23]

Mwanamke mmoja siku moja katika mkutano wa mitaani alisema, "Yesu alimuomba nani pale bustani ya Gethsemane,?"

Nikasema, "Napenda nikuulize jambo fulani, ulishuhudia kwamba una Roho Mtakatifu. Yuko wapi? Unamuomba nani? tunajua yuko ndani yako.

Vema, tunae Roho Mtakatifu kwa kipimo. Alikuwa Naye bila kipimo. Tuna wana na binti za Mungu kwa kipimo, (2korintho10:13; warumi12:3). Kama kuchukuwa kijiko kilichojaa maji kutoka baharini. Ni ule uwingi lakini thamani yake ni moja. Kwa hiyo kama Yesu Kristo ni yule jana leo na hata

milele (Waebrania 13:8). Mungu ndani yetu. Ndio.
[24]

Bwana Yesu, tunanyenyekea kuja kwako tukikiri makosa yetu. Tunakuja tukikiri kwamba tumestahili magonjwa na kifo na huzuni, lakini tunaukubali upatanisho wako kwa dhambi zetu na magonjwa yetu (Yohana3:14-15). Na usiku wa leo hawa wana na binti za Mungu wamekaa hapa, na kusikia masahihisho ya Neno na kuinua mikono yao, na kutaka kutembea karibu na wewe. Ulisema maombi ya Imani yatamuokoa mgonjwa na Mungu atamwinua:Na hata kama ametenda dhambi atasamehewa. Ungamianeni ninyi kwa ninyi ombeaneni mmoja kwa mwingine mpate kuponywa. Kwa maana maombi ya mwenye haki yafaa sana akiomba kwa bidii (Yakobo 5:16). [25].

Nukuu za kiingereza

[1] Uchungu wa kuzaa uk.5
[2] "Imani" Aya. E-5
[3] Imani waliokabidhiwa watakatifu uk.E-8
[4] maswali& majibu kum uk.1162 s-398
[5] "kuhesabu kinyumenyume" Aya12-14
[7] "Ishara ya kweli isiyo tazamwa" Aya1116
[8] "Unasema huyu ni nani? Aya55-57
[9] Ishara ya kweli isiyo tazamwa Aya186
[10] Msingi wa asili wa Imani Aya16-17
[11] Kristo akifunuliwa katika Neno lake Aya33-35
[12] "kwa nini" AyaE-86
[13] Natumuone Mungu Aya:196
[14] Maswali & majibu, kum pg1162,5-397
[15] Ufunuo sura ya 4seh.1. Aya43
[16] "Onyo halafu hukumu"Aya10
[17] Hekima vs Imani uk.52
[18] Roho zidanganyazo Aya42-45
[19] Ufunuo kitabu cha Alama Aya35-42;48
[20] Shitaka, uk.3
[21] Kuondoa presha Aya276
[22] Shitaka uk.43
[23] Ile mbegu haitarithi na kapi Aya126
[24] Tuonyeshe baba Aya E.68b-E69
[25] Mambo yatakayokuwa Aya153.

*jiwe la kiroho la kujengea na 167 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebeievers.de*



*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.*
*(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*